# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

PARLIAMENT OF TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2020—2025)

## TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2024/2023
## VOLUME VI

**JUNI 30, 2024**

**YALIYOMO**

1. YALIYOMO……………………..……………...1

2. UTANGULIZI…………………………………….. 2

3. MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020-2025
*(TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2024/2023)*

3.1 MIRADI YA ELIMU…………………………. 5

3.2 MIRADI YA AFYA…………………………….. 45

3.3 MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI…. 55

3.4 MIRADI YA MAJI……………………………….. 63

3.5 MIRADI YA UJENZI WA BARABARA……….. 69

3.6 UTAMADUNI NA MICHEZO ………………….. 73

4. MENGINEYO……………………………………. 77

5. HITIMISHO………………………………………. 96

6. SHUKRANI……………………………………. 98

## UTANGULIZI

Kitabu hiki ni moja ya chapisho linalotoa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kuanzia Mwaka 2020 hadi 2025

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, ameweka utaratibu wa kuchapisha vitabu vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani za Uchaguzi za CCM ndani ya Jimbo lao kama ifuatavyo:

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020:**

Vitabu viwili (2) vilichapishwa:

(i) Julai 7, 2019 (Volume I)

(ii) June 30, 2020 (Volume II)

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025:**

Machapisho ya utekelezaji wa Ilani hii ya Uchaguzi yameanza kutolewa kwenye vitabu kama ifuatavyo:

(iii) Juni 30, 2021 (Volume III)

(iv) Juni 30, 2022 (Volume IV)

(v) Juni 30, 2023 (Volume V)

(vi) Juni 30, 2024 (Volume VI)

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374. Jimbo letu limechagua vipaumbele vitano kutoka ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025.

Vipaumbele hivyo ni: (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, (iv) Tabianchi na Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni.

Maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, rasilimali watu, na taasisi za fedha na uchumi ni nyenzo muhimu zinazohitajika kufanikisha utekelezaji wa miradi inayoibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano.

Wanavijiji kwa kushirikiana na viongozi wao wa ngazi mbalimbali hupendekeza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji yao, na huchangia nguvukazi na mali zao kwenye utekelezaji wa miradi ya chaguo lao. Uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wanavijiji unafuata taratibu na sheria zilizowekwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan inapongezwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea kuboresha na kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi wa Jimbo hili.

Kitabu hiki (Volume VI) ni chapisho linaloelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023). Vilevile, taarifa hii inaonesha michango mingi na mikubwa iliyotolewa na Serikali Kuu, Mbunge wa Jimbo, Wanavijiji, baadhi ya Wazaliwa wa Jimboni mwetu, na Wadau wengine wa maendeleo ya Musoma Vijijini.

Kitabu hiki, kama vilivyo vingine vyote vya taarifa za maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini hugawiwa bure. Haviuzwi!

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI YA ELIMU

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# KISIWA CHA RUKUBA CHADHAMIRIA KUFUNGUA SEKONDARI YAKE MWAKANI (JANUARI 2025)

July 1, 2024



Kisiwa cha Rukuba cha Jimbo la Musoma Vijijini kimedhamiria kukamilisha miundombinu ya elimu ya awali ya kukiwezesha kuwa na sekondari yake ifikapo Januari 2025.

Kisiwa hiki kinayo Shule ya Msingi moja yenye maktaba na nyumba za walimu za kutosheleza mahitaji yao.

Vilevile, Kisiwa hiki kimechangiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali yetu kukamilisha Kituo cha Afya hapo Kisiwani. Sasa kinajenga sekondari yake

**Ujenzi wa Rukuba Sekondari:**
Ujenzi ulianza kwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo kwenda hapo Kisiwani kuhamasisha na kuanza kuchangia ujenzi kupitia Harambee aliyoipiga hapo Kisiwani.

Michango ya awali ya kuanza ujenzi imetolewa na wafuatao:

**(i) Wakazi wa Kisiwa cha Rukuba na Wadau wao wa Maendeleo:**

*Fedha taslimu: Tsh 1,708,000
*Saruji Mifuko 72
*Kokoto: Tsh 804,000
*Fedha za Fundi: Tsh 2,300,000
*Fundi wa Matofali: Tsh 500,000
*Nondo
*Nguvukazi: mchanga, maji, kuchimba msingi.

**(ii) Viongozi wa Wilaya:**

*DC Dkt Khalfany Haule: Tsh 500,000
*DED Nitu Palela: Saruji Mifuko 20

**(iii) Mbunge wa Jimbo**

*Saruji Mifuko 150 (bado 50)
*Saruji Mifuko 205 (Mfuko wa Jimbo)

**Ujenzi wa Sekondari mpya Jimboni mwetu:**

Jimbo letu lenye Kata 21 zenye jumla ya vijiji 68, lina jumla ya Sekondari 28 (26 za Kata na 2 za Binafsi).

i.) **Sekondari mpya zinazojengwa kwa wakati huu vijijini mwetu (4):**

Nyasaungu, Muhoji, Kisiwani Rukuba na Kurwaki. Muhoji imeanza kupokea fedha kutoka Serikalini Tsh milioni 75 (Tsh 75m) - tunajitahidi sekondari hizi zote zifunguliwe mwakani (Januari 2025)

ii.) **Ujenzi wa Sekondari mpya kwa kutumia fedha za Serikali Kuu utaanza hivi karibuni.**

Kata ya Nyamrandirira (Kijijini Kasoma) na Kata ya Bukima (Kijijini Butata). Hizi zitafunguliwa Januari 2025.

iii.) **Ujenzi wa Maabara:**

Ujenzi maabara 3 za masomo ya sayansi kwa kila Sekondari ya Kata unaendelea. Ujenzi huu unafanikishwa kwa michango kutoka Serikalini, na kutoka kwa wanavijiji na viongozi wao.

iv.) **Sekondari mpya zitakazoanzwa kujengwa kwa kutumia Michango ya wananchi (4):**

Wanavijiji wamemuomba Mbunge wao wa Jimbo akapige Harambee za kuanza ujenzi wa sekondari mpya kwenye vijiji vifuatavyo: Mmahare, Kiriba, Kataryo na Chitare. Kazi hii amekubali kuifanya (Julai-Agosti 2024)

**Michango kutoka kwa Wazaliwa na Musoma Vijijini na Wadau wetu wa Maendeleo:**

Tunaombwa tuanze na tuendelee kuchangia maendeleo na ustawi wa ndugu zetu wa Musoma Vijijini - karibuni tuungane pamoja kivitendo!

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# BULINGA SEKONDARI KUKAMILISHA MAABARA YA FIZIKIA MWEZI AGOSTI 2024

April 16, 2024



*Wanafunzi wa Bulinga Sekondari wakiwa kwenye kipindi cha mafunzo kwa vitendo (practicals) ndani ya Maabara yao ya Kemia.*

Jimbo la Musoma Vijijini lina mradi kabambe wa ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi (fizikia, kemia na baiolojia) kwenye Sekondari zake zote za Kata. Wananchi na Serikali yetu wanashirikiana vizuri sana kwenye utekelezaji wa mradi huu.

Jimbo hili lina Sekondari za Kata 26 na wanavijiji wanajenga nyingine 10. Sekondari za Binafsi ni mbili (2).

Bulinga Sekondari ni ya Kata ya Bulinga yenye vijiji vitatu (3) ambavyo ni: Bujaga, Bulinga na Busungu. Ilianza kutoa elimu ya masomo ya sekondari Mwaka 2016, na kusajiliwa rasmi Mwaka 2019.

Bulinga Sekondari inazo maabara mbili (2) za masomo ya kemia na bailojia ambazo zinatumika. Maabara moja ya somo la fizikia hakijakamilishwa.

Sekondari hii yenye wanafunzi 610 ilitembelewa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, kwa lengo la kufuatilia ustawi wake na kupokea orodha ya mapungufu ya shule hii. Hiyo ilikuwa tarehe 12.4.2024

Vilevile, Mbunge huyo aliwakaribisha wananchi kutoka vijiji vitatu vya Kata ya Bulinga kwa lengo la kupokea na kutatua matatizo na kero zao.

Wananchi hao waligawiwa vitabu viwili viwili (Volumes III&IV) vinavyoelezea mafanikio makubwa yanayopatikana kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 ndani ya Jimbo letu.

**Ukamilishaji wa Maabara ya Fizikia:**
Kikao cha Mbunge wa Jimbo wa Jimbo, wananchi wa Kata ya Bulinga, walimu na baadhi ya wanafunzi wa Bulinga Sekondari kiliazimia yafuatayo:

i.) Maabara ya Fizikia iliyojengwa hadi usawa wa renta ikamilishwe kabla ya tarehe 30.8.2024

ii.) Mabati ya rangi 120 yanayohitajika:
* Kila kijiji kichangie mabati 24, jumla mabati 72
* Mbunge wa Jimbo achangie mabati 24
* Halmashauri yetu ichangie mabati 24

iii.) Mbao na misumari
Wanavijiji na Mbunge wao wamejiwekea utaratibu wa kununua vifaa hivi vya ujenzi.

Michango yote iliyoainishwa hapo juu iwasilishwe kwa Mkuu (Headmaster) wa Bulinga Sekondari ifikapo tarehe 15.8.2024.
Michango kutoka kwa Wana-Bulinga na Wadau wengine wa maendeleo:

i.) **Wanaopenda kuchangia vifaa vya ujenzi:**
Wanaombwa waviwasilishe kwa Mkuu (Headmaster) wa Bulinga Sekondari.

ii.) **Michango ya fedha ipelekwe kwenye Akaunti ya Shule ambayo ni:**
Benki: NMB
Akaunti Na: 30310029434
Jina: Bulinga Secondary School

**KARIBUNI TUKAMILISHE UJENZI WA MAABARA YA FIZIKIA YA BULINGA SEKONDARI**

Boma la Maabara ya Fizikia linalohitaji ukamilishwaji.

Mbunge wa Jimbo alikabidhi Saruji Mifuko 100 ya ukamilishaji wa maabara hiyo.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# NYANJA SEKONDARI YAAMUA KUANZA UJENZI WA MAABARA TATU ZA MASOMO YA SAYANSI

April 12, 2024



*Mbunge wa Jimbo akikabidhi saruji ya ujenzi wa maabara tatu (3) za masomo ya sayansi ya Nyanja Sekondari ya Kata ya Bwasi. Wananchi wakiwa wamegawiwa vitabu viwili viwili (Volumes III & IV) vinavyoelezea mafanikio makubwa yanayopatikana kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 ndani ya Jimbo letu.*

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 lina jumla ya Vijiji 68 na Vitongoji 374.

Jimbo hili lina Sekondari 28, kati ya hizo 26 ni za Kata/Serikali na 2 ni za Binafsi (private). Wanavijiji wanajenga sekondari nyingine 10.

**Nyanja Sekondari: miundombinu ya elimu:**
Sekondari hii ni ya Kata ya Bwasi yenye vijiji vitatu (3) vya Bugunda, Bwasi na Kome. Ilifunguliwa Mwaka 2006, ina wanafunzi 495 na walimu 11.

Sekondari hii haina maabara hata moja, haina jengo la utawala na ina upungufu wa vyumba vinne vya madarasa. Kuna nyumba moja tu ya walimu.

**Maabara 3 kujengwa ndani ya miezi 4:**
Kikao kilichohudhuriwa na baadhi ya wanavijiji, viongozi wa Chama na Serikali wa Kata ya Bwasi na Mbunge wa Jimbo kiliazimia kwamba ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi (physics, chemistry and biology) uanze mara moja na maboma yawe yamekamilika ifikapo tarehe 15.8.2024.

Mbunge wa Jimbo atarudi shuleni hapo kukagua ujenzi huo.

**Upatikanaji wa vifaa vya ujenzi:**
Harambee ya Mbunge wa Jimbo iliyopigwa Septemba 2023 iliwezesha kupatikana kwa:

*Saruji Mifuko 41 kutoka kwa wananchi
*Tsh 549,000
*Saruji Mifuko 100 za Mbunge wa Jimbo.

Hata hivyo ujenzi haujaanza kwa sababu mbalimbali ambazo ziko mikononi mwa Serikali ya Kata na vijiji vyake vitatu!

**Mchango wa Mfuko wa Jimbo:**
Saruji Mifuko 100 imegawiwa kwenye shule hii.

**Michango kutoka kwa Wana-Bwasi na Wadau wengine wa Maendeleo:**

*Michango ya vifaa vya ujenzi ipelekwe kwa Mkuu wa Shule
*Michango ya fedha ipelekwe moja kwa moja kwenye Akaunti ya Shule ambayo ni:

Benki: NMB
Akaunti Na: 30301200349
Jina: Nyanja Sekondari

**WANA-BWASI TUJITOKEZE KUCHANGIA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA SEKONDARI YA KATA YETU**

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# ETARO SEKONDARI INAJENGA MIUNDOMBINU YA ELIMU INAYOHITAJIKA KUANZISHA “HIGH SCHOOL” YA MASOMO YA SAYANSI

April 8, 2024



*Wanafunzi wa Etaro Sekondari wakiwa kwenye masomo ya vitendo (practicals) ndani ya Chumba cha Kompyuta.*

Idadi ya shule ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye jumla ya vijiji 68 ni kama ifuatavyo:

*Shule za Msingi 120: 116 (Serikali) na 4 (Binafsi). Shule Shikizi 13 (ujenzi unaendelea)

*Sekondari 28: 26 (Kata/Serikali) na 2 (Binafsi). 10 mpya (zinajengwa na wanavijiji)

**Etaro Sekondari:**
Ilifunguliwa Mwaka 2006, ina jumla ya wanafunzi 897 kutoka vijiji vinne vya Kata ya Etaro.

**Maabara za Kemia & Baiolojia:**
Sekondari hii inazo MAABARA MBILI zilizokamilika na zinatumika. Hizo ni maabara za masomo ya Kemia na Baiolojia.

**Maabara ya Fizikia:**
Maabara ya Fizikia (boma lipo) itakamilishwa ifikapo tarehe 30.4.2024 kwa kutumia vifaa vilivyonunuliwa kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo la Musoma Vijijini. Mbunge wa Jimbo ameikabadhi sekondari hiyo MABATI ya RANGI 120, SARUJI MIFUKO 100 na NONDO 40 kwa ajili ya ukamilishaji wa Maabara hiyo.

**Chumba cha Kompyuta:**
Kompyuta ishirini na tano (25) zimenunuliwa na rafiki wa Etaro Sekondari ambae ni Northern Illinois University, USA. Chuo hiki kilianzishwa tarehe 22.5.1895

**Lengo la kuanzisha "High School" ya sayansi**
Kwenye kikao cha hivi karibuni cha Mbunge wa Jimbo na wananchi wa Kata ya Etaro, moja ya maazimio muhimu yaliyofanyika ni uanzishwaji wa "high school" ya masomo ya sayansi, yakiwemo ya "computer science" kwenye sekondari hii.

Imepangwa kwamba Mwezi Julai 2024, Mbunge wa Jimbo ataendesha Harambee ya ujenzi wa mabweni, bwalo la chakula, n.k. ikiwa ni baadhi ya miundombinu muhimu inayohitajika kwa ajili ya uanzishwaji wa "high school"

**PONGEZI:**
Serikali yetu inapongezwa kwa kutoa michango mbalimbali ya ustawi wa Etaro Sekondari tokea Mwaka 2006.

Wananchi wa Kata ya Etaro, hasa wazazi wa wanafunzi wa Etaro Sekondari wanapongezwa sana kwa kukubali kwao kuendelea kuchangia maendeleo ya sekondari yao.

Walimu, chini ya uongozi mzuri wa Mkuu wa Shule, Mwl Jacob Joseph Chagavalye wanapongezwa sana kwa ubunifu wao.

Rafiki zetu wa Marekani, Northern Illinois University nao wanapongezwa sana kwa uwezeshaji wao wa kutupatia na kutufungia mtandao wenye Kompyuta 25 hapo shuleni.

**TUENDELEE KUCHANGIA UBORESHAJI NA UPANUZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWENYE SHULE ZETU ZA MUSOMA VIJIJINI**

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# WANAKIJIJI WAANZA UJENZI WA "DAVID MASSAMBA MEMORIAL SECONDARY SCHOOL"

March 28, 2024



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo akiwa na wanakijiji wa Kurwaki kwenye eneo la ujenzi wa, "David Massamba Memorial Secondary School." Hiyo ilikuwa Jumatano, 20.3.2024.*

Wakazi wa Kijiji cha Kurwaki, Kata ya Mugango wameanza ujenzi wa "David Massamba Memorial Secondary School."

Sekondari hii ambayo itakuwa ya pili kwa Kata ya Mugango inajengwa ikiwa imepewa jina la Marehemu Prof David Massamba, mzaliwa wa Kijiji cha Kurwaki, na aliyekuwa bingwa wa mabingwa wa Lugha ya Kiswahili.

Kazi kubwa za ustawishaji wa Lugha ya Kiswahili zilizofanywa na Marehemu Prof David Massamba, kwa kushirikiana na Wataalamu wenzake, ni pamoja na:

*Kuandika vitabu vinavyotumika Vyuo Vikuu na Sekondari (Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu).

*Uandishi wa Kamusi ya Kiswahili

**Michango ya awali ya ujenzi:**
(i) Wanakijiji: Tsh 1,870,000
(ii) Familia Massamba: Tsh 800,000
(iii) Wazaliwa 2 wa Kurwaki: Tsh 750,000
(Dr Rukonge Manoko & Ndg Kawawa Jackson)
(iv) Diwani wa Kata: Tsh 200,000
(v) Wazazi wa Kijiji jirani, Kiriba: Tsh 80,000
(vi) Walimu Makada: Tsh 70,000

**Michango ya Mbunge wa Jimbo:**
(i) Binafsi: Saruji Mifuko 250
(ii) Mfuko wa Jimbo: Saruji Mifuko 205

**Akaunti ya Kijiji ya kutuma michango:**
**Benki: NMB**
Akaunti Na: 30302301539
Jina: Kijiji cha Kurwaki

Tafadhali tunaomba tuendelee kuchangia ujenzi wa Sekondari hii ambayo itakuwa ni kumbukumbu nzuri ya kuenzi kazi nyingi na muhimu sana alizozifanya Marehemu Prof David Massamba kwenye ukuzaji na usitawishaji wa Lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UHURU NA KAZI – DHAMIRA YA KIJIJI CHA MUHOJI KUFUNGUA SEKONDARI YAKE MWAKANI IKO PALE PALE

**December 11, 2023**



*Wanakijiji wakilima barabara ya kuingia shuleni (Muhoji Sekondari)*

**UHURU NA KAZI - DHAMIRA YA KIJIJI CHA MUHOJI KUFUNGUA SEKONDARI YAKE MWAKANI IKO PALE PALE**

Wananchi wa Kijiji cha Muhoji, Kata ya Bugwema wameamua kujenga Sekondari yao (Muhoji Sekondari) na dhamira ya kuifungua shule hiyo Januari 2024 iko pale pale.

**Ujenzi wa awali unaokamilishwa ni:**

*Vyumba 2 vya madarasa

*Ofisi 1 ya walimu

**Vyoo:**

Matundu 12 ya wasichana
Matundu 12 ya wavulana
Matundu 2 ya walimu

*Barabara ya kuingia shuleni kutoka barabara kuu (nguvukazi za wanakijiji)

**Wachangiaji wakuu wa ujenzi wa Muhoji Sekondari ni:**

*Wananchi wa Kijiji cha Muhoji
*Mbunge wa Jimbo
*Mfuko wa Jimbo
*Wazaliwa watatu (3) wa Kijiji cha Muhoji

Halmashauri yetu (Musoma DC) bado haijachangia cho chote.

TARURA imeombwa isaidie ukamilishaji wa ujenzi wa barabara linaloingia Muhoji Sekondari likitokea barabara kuu la Murangi-Masinono-Manyamanyama (Bunda).

Muhoji Sekondari itakuwa ni Sekondari ya pili ya Kata ya Bugwema yenye vijiji vinne (Bugwema, Kinyang'erere, Masinono na Muhoji).

Sekondari moja (Bugwema Sekondari) kwa Kata hii haitoshi, matatizo makuu yakiwa ni umbali mrefu wa kutembea kwa baadhi ya wanafunzi, na mirundikano madarasani.

**Ombi kutoka Kijijini Muhoji:**

*Wazaliwa au watu wenye chimbuko la Kata ya Bugwema wanaombwa waungane na ndugu zao kukamilisha ujenzi wa Muhoji Sekondari.

*Wadau wengine wa maendeleo wanaombwa sana wachangie ujenzi wa shule hii.

**Michango ya fedha ipelekwe:**
Benki: NMB
Akaunti Na: 30302301062
Jina la Akaunti: Serikali ya Kijiji cha Muhoji

**Picha zilizoambatanishwa hapa (Ukurasa 23):**
*Jengo lenye Vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu
*Wanakijiji wakijenga vyoo vya shule (Muhoji Sekondari)

**UHURU NA KAZI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz



*Jengo lenye vyumba 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya walimu*



*Wanakijiji wakijenga vyoo vya shule (Muhoji Sekondari)*

# UJENZI WA MAABARA TATU ZA MASOMO YA SAYANSI KWENYE SEKONDARI YA MTIRO UNAENDELEA VIZURI

November 22, 2023



*Picha hii inaonesha maendeleo ya ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi kwenye Sekondari ya Mtiro ya Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini*

Maendeleo ya ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi kwenye Sekondari ya Mtiro ya Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini ni mazuri.

Rejea taarifa yetu ya Jumatatu, 6.11.2023 kuhusu umuhimu wa kujenga maabara tatu za masomo ya sayansi kwenye Sekondari ya Mtiro ya Kata ya Bukumi.

Ujenzi wa aina hii unafanyika kwenye Sekondari zote za Jimbo la Musoma Vijijini (25 za Kata/Serikali na 2 za Binafsi za Madhehebu ya Katoliki & SDA).

Wanavijiji wa Kata ya Bukumi (Vijiji vya Buira, Bukumi, Buraga na Busekera) wanaendelea kuchangia ujenzi huu.

*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo nae anaendelea kuchangia ujenzi huu. Juzi ameongeza mchango wake kwa kuwapatia Saruji Mifuko 50 (hamsini).

*Matofali ya ujenzi huu yanaendelea kufyatuliwa kwenye eneo la ujenzi na kila mfuko mmoja wa saruji unatoa matofali 25 - ubora unaokubalika.

*Wanavijiji wanaomba mchango wako, na tafadhali upeleke kwenye Akaunti ya Benki ya Sekondari hiyo ambayo ni:

Jina la Akaunti:
Mtiro Secondary School
Benki (Musoma):
NMB
Akaunti Namba:
30301200299

Tunatanguliza shukrani zetu za dhati.

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# UJENZI WA SEKONDARI MPYA UNAENDELEA MUSOMA VIJIJINI: KISIWA CHA RUKUBA KIMEANZA UJENZI WA SEKONDARI YAKE

November 3, 2023



*Mwanzo wa ujenzi wa Sekondari ya Kisiwa cha Rukuba - ujenzi wa msingi wa mawe wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu.*

Jimbo la Musoma Vijijini lina Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374.

Jimbo hili lina jumla ya Sekondari:
*25 za Kata (Serikali)
*2 za Binafsi (Katoliki & SDA)

Sekondari mpya tano (5) zinajengwa kwenye vijiji vitano - Kisiwa cha Rukuba (Kata ya Etaro), Nyasaungu (Kata ya Ifulifu), Kurwaki (Kata ya Mugango), Muhoji (Kata ya Bugwema), na Wanyere (Kata ya Suguti, serikali inagharamia ujenzi).

**Sekondari ya Kisiwa cha Rukuba**
Wakazi wa Kisiwa cha Rukuba wameamua kujenga sekondari yao ili elimu ya sekondari itolewe hapo Kisiwani badala ya wanafunzi kwenda kupanga vyumba nchi kavu (Kijijini Etaro) kwa ajili ya elimu yao ya sekondari.

Harambee ya kwanza ya ujenzi wa Sekondari ya Kisiwa cha Rukuba ilishafanyika chini ya usimamizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, akishirikiana na Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Musoma Vijijini.

**Ujenzi umeanza**
*Matofali 2,900 tayari yametengenezwa: kila mfuko mmoja (1) wa saruji umetoa matofali 25

*Ujenzi wa vyumba viwili na ofisi moja ya walimu umeanza - msingi wa mawe unajengwa (angalia picha ya hapa Ukurasa wa 26)

**Tafadhali sana tunaomba mchango wako**:
*Akaunti ya kuweka mchango wako wa fedha ni:
Benki: NMB
Akaunti Namba: 30302300701
Jina la Akaunti:
Serikali ya Kijiji cha Rukuba

Wakazi wa Kisiwa cha Rukuba wamedhamiria kujenga Sekondari kisiwani humo ili kuboresha upatinakaji wa elimu ya sekondari kwa watoto wao - tuwaunge mkono.

**Mchango wa Mbunge wa Jimbo**
*Prof Sospeter Muhongo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini ameishachangia Saruji Mifuko 100
*Mbunge huyo anatoa tena Saruji Mifuko 50, itakayochukuliwa

leo, na ataendelea kuchangia ujenzi huo.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SEKONDARI ILIYOFUNGULIWA MWAKA 2006 YAAMUA KUANZA KUJENGA MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI

October 14, 2023



*Pichani ni Harambee ya jana iliyofanyika Nyanja Sekondari, Kijijini Kome, Kata ya Bwasi*

Sekondari hii iliyofunguliwa mwaka 2006 yaamua kuanza kujenga maabara za masomo ya sayansi

Nyanja Sekondari ni ya Kata ya Bwasi yenye vijiji vitatu (3) vyenye jumla ya vitongoji ishirini na vitatu (23). Vijiji hivyo ni Bugunda, Bwasi na Bugunda.

Sekondari hii kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 547, na walimu 12 wenye ajira, na 5 wa kujitolea.

**Harambee ya ujenzi wa maabara:**
Sekondari haina maabara hata moja na mwitikio wa wanafunzi kusoma masomo ya sayansi ni mdogo sana

Kwa mfano, Kidato cha Nne (Form IV) chenye jumla ya wanafunzi 96, ni wanafunzi 13 tu wanaosoma somo la Fizikia.

*Jana, Jumatatu, 9.10.2023, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini na Kamati ya Siasa ya Wilaya (CCM) waliendesha HARAMBEE ya kuanza ujenzi wa maabara za Fizikia, Kemia na Baiolojia za sekondari hiyo.

**Mapato ya Harambee:**
*Fedha: Tsh 1,105,000
*Saruji Mifuko 141(ikiwemo Mifuko 100 ya Mbunge wa Jimbo)

**Kamati ya Ujenzi:**
Kamati ya Ujenzi ya watu wanne (4) imeundwa.

**KARIBUNI TUCHANGIE UJENZI WA MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI KWENYE SEKONDARI ZA KATA ZA MUSOMA VIJIJINI**

**Idadi ya Sekondari Jimboni (Kata 21) mwetu:**
*25 za Kata

*2 za Binafsi
*5 zinajengwa

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

## WANANCHI WA KATA YA NYEGINA WAAMUA KUHARAKISHA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SEKONDARI YAO MPYA

April 2, 2024



*Mkutano wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, na wananchi wa Kata ya Nyegina, wakiwemo walimu na wanafunzi wa Bukwaya Sekondari, na wanafunzi wa Shule ya Msingi Nyegina. Hii ilikuwa siku ya Alhamisi, 28.3.2024*

Kata ya Nyegina yenye vijiji vitatu (Kurukerege, Mkirira na Nyegina) inazo sekondari mbili ambazo ni Mkirira na Bukwaya. Sekondari ya Bukwaya ni mpya, ilifunguliwa Julai 2022.

**Uharakishaji wa ujenzi wa miundombinu ya Bukwaya Sekondari:**

Sekondari hii ina mapungufu mengi na wanavijiji wa Kata ya Nyegina wameamua kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya shule yao.

Uamuzi huo ulifanywa kwa kumshirikisha Mbunge wao, Prof Sospeter Muhongo alipotembelea shule hiyo siku ya Alhamisi, 28.3.2024

**Tarehe 30.4.2024:**
Ifikapo tarehe hii, vyumba viwili vya madarasa ambavyo tayari vimeezekwa vitakuwa vimekamilishwa. Mbunge wa Jimbo amewakabidhi Saruji Mifuko 150 iliyonunuliwa kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo.

**Tarehe 30.5. 2024:**
Ifikapo tarehe hii, matundu sita (6) ya choo yatakuwa yamekamilika

**Mwezi Julai 2024:**
Mbunge wa Jimbo atapiga Harambee ya kuanza ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi, ambayo ni fizikia, kemia na bailojia.

**Michango ya ujenzi wa Bukwaya Sekondari:**
Sekondari hii alianza kujengwa kwa nguvu za wananchi na Mbunge wa Jimbo. Orodha ya michango yote imetunzwa shuleni hapo.

Serikali inashukuliwa sana kwa kuchangia Tsh Milioni 40 (arobaini) zikiwa ni fedha za UVIKO.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# HARAMBEE IMEFANIKIWA SANA: KISIWA CHA RUKUBA CHAANZA UJENZI WA SEKONDARI YAKE

September 30, 2023



**HARAMBEE IMEFANIKIWA SANA: KISIWA CHA RUKUBA CHAANZA UJENZI WA SEKONDARI YAKE**

Kisiwa cha Rukuba ni moja ya vijiji vinne (4) vya Kata ya Etaro. Wanafunzi wa sekondari kutoka Kisiwani humo wanasoma nchi kavu kwenye sekondari ya Kata yao (Etaro Sekondari).

Wanafunzi hao wanakumbuna na matatizo mengi mno ambayo yanadhoofisha sana maendeleo yao kielimu. Kwa hiyo, wakazi

wa Kisiwa cha Rukuba wameamua kujenga sekondari yao Kisiwani humo.

**Harambee yenye mafanikio makubwa**
Harambee iliyoendeshwa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini siku ya Jumatano, 27.9.2023 ilishirikisha Viongozi wote wakuu wa Wilaya ya Musoma na Halmashauri yake (Musoma DC).

Wafanyakazi wa kada mbalimbali, wakiwemo Walimu Makada ya CCM walishiriki. Kamati ya Siasa ya Wilaya CCM nayo ilishiriki - ilikuwa ni Harambee ya kipekee kufanyika Kisiwani humo.

**Michango iliyopatikana kwenye Harambee hiyo**
*Wakazi na Wazaliwa wa Kisiwa cha Rukuba:
  Saruji Mifuko 167
*Kamati ya Siasa ya Kata (CCM):
  Saruji Mifuko 22
*Kamati ya Siasa ya Wilaya (CCM):
  Saruji Mifuko 15
*DED na wenzake: Saruji Mifuko 20
*DC na wenzake: Saruji Mifuko 62
*Mbunge wa Jimbo: Saruji Mifuko 200
*Fedha taslimu: Tsh 248,000
  (zikiwemo Tsh 105,000 za Walimu Makada wa CCM)

Karibuni tujenge Sekondari ya Kisiwa cha Rukuba cha Musoma Vijijini.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini

# WANAVIJIJI WAENDELEA KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUJENGA MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI KWENYE SEKONDARI ZAO ZA KATA

July 4, 2023



*Wanafunzi wa Kiriba Sekondari wakiwa wanafanya mazoezi kwenye Maabara yao ya Kemia (Chemistry practical class)*

Wanavijiji wa Jimbo la Musoma Vijijini wamedhamiria kujenga MAABARA TATU za masomo ya sayansi kwenye Sekondari zao za Kata. Maabara hizo ni za masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia.

Jimbo letu lenye Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374 lina jumla ya Sekondari 25 za Kata, na 2 za Binafsi (Katoliki & SDA).

**Vyanzo vya michango ya ujenzi wa maabara hizo ni:**
*Michango ya fedha taslimu kutoka kwa Wanavijiji na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo

*Nguvukazi za Wanavijiji - kusomba mawe, kokoto, mchanga, maji na kuchimba misingi ya majengo

*Fedha za Mfuko wa Jimbo

*Fedha kutoka Serikali Kuu, yaani TAMISEMI na Wizara ya Elimu

*Wadau wa Maendeleo zikiwemo Benki za NMB, CRDB, NBC na POSTA.

*Baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini

**Sekondari zenye Maabara 3 za Masomo ya Sayansi zilizokamilika na zinazotumika ni:**

(i) Mugango, Kata ya Mugango, (ii) Bugwema, Kata ya Bugwema, (iii) Kiriba, Kata ya Kiriba, (iv) Nyakatende, Kata ya Nyakatende, na (v) Ifulifu, Kata ya Ifulifu, (vi) Makojo

Sekondari ya Kata ya Makojo, itakamilisha maabara ya tatu kabla ya tarehe 30.7.2023

Sekondari nyingine 19 za Kata zinaendelea na ujenzi wa Maabara 3, na lengo ni kukamilisha ujenzi huo mwakani, kabla ya Julai 2024.

Sekondari 4 mpya zinazojengwa (Nyasaungu, Muhoji, Wanyere na Rukuba Kisiwani) lazima majengo ya maabara 3 za masomo ya sayansi yawe sehemu ya ujenzi wa sekondari hizo.

Halmashauri yetu (Musoma DC) inaendelea kushawishiwa na kuombwa nayo ianze kuchangia, kwa kutumia mapato yake ya ndani, ujenzi wa Maabara na Maktaba kwenye shule zetu!

**Musoma Vijijini inaomba ipewe "High Schools" za Masomo ya Sayansi:**

*Sekondari 6 zilizotajwa hapo juu ziko tayari kuanza kupokea Wanafunzi wa Form V (Kidato cha V) mwakani, Julai 2024.

Masomo ya Hisabati na Sayansi kwa ngazi ya awali ya shule za msingi na sekondari ndiyo msingi imara wa taaluma mbalimbali za kiufundi zinazotoa, kwa uharaka, ajira ndani na nje ya nchi.

**SHUKRANI**
Wanafunzi wa Sekondari za Kata za Musoma Vijijini, Wazazi na Viongozi wao wa ngazi zote, wanaishukuru Serikali yetu chini ya uongozi mzuri wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuchangia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya elimu Jimboni mwetu - Ahsante sana.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# HARAMBEE YA MBUNGE YAFANIKISHA UPAUAJI WA MADARASA YA SHULE SHIKIZI KIUNDA YA MUSOMA VIJIJINI

January 17, 2024



*Wakazi wa Kitongoji cha Kiunda na Viongozi mbalimbali wakiwa kwenye Harambee iliyofanyika kwenye eneo la ujenzi wa Shule Shikizi Kiunda ya Kijijini Kamguruki, Kata ya Nyakatende, Musoma Vijijini.*

Tarehe 12.1.2024, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo aliendesha HARAMBEE iliyolenga

kukamilisha kazi ya upauaji wa boma la Shule Shikizi Kiunda ya Kijijini Kamguruki, Kata ya Nyakatende.

Boma hilo (picha imeambatanishwa hapa) ni la vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu. Boma limejengwa kwa michango ya Wana-Kitongoji cha Kiunda, Diwani wa Kata na Mbunge wa Jimbo.

**Ujenzi wa Shule Shikizi Jimboni mwetu**
Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye vijiji 68 na vitongoji 374 ina shule za msingi zenye idadi ifuatayo:
*111 shule za Serikali
*4 shule Binafsi
*12 shule shikizi zinazopanuliwa

**Harambee ya Shule Shikizi Kiunda**
*Gharama zote za upauaji:
Tsh 4,268,000

***Fedha zilizopatikana kwenye Harambee:**
Tsh 1,285,000.

**Wachangiaji:**
(i) Wakazi wa Kijiji cha Kamguruki
(ii) Wakazi kutoka Vijiji jirani
(iii) DEO Hamisi Shemahonge
(iv) Viongozi wa Chama Wilaya & Jumuiya zake ambao ni Ndg Jackson Nyakia, Ndg William Magero, Ndg Bwire Mkuku na Ndg Sophia Maregesi.

***Mabati yaliyopatikana kwenye Harambee:**
(i) Ndg Pascal Maganga: Mabati 24
(ii) Diwani Mhe Kisha Marere: Mabati 36
(iii) Mbunge Prof Muhongo: Mabati 72

**Ratiba ya upauaji**
*Tarehe 23.2.2024
Mbao za paa (kenji) zianze kuwekwa

*Tarehe 24.2.2024
Mabati yaanze kuwekwa (kuezeka)

Kaimu Mtendaji wa Kijiji (VEO), Ndg Magreth Malima anapewa pongezi nyingi za usimamiaji mzuri wa shughuli za maendeleo ndani ya Kijiji cha Kamguruki

**MICHANGO INAKARIBISHWA SANA**
Wana-Kitongoji cha Kiunda, na Kata ya Nyakatende kwa ujumla wanaendelea kuomba michango kutoka vyanzo mbalimbali ili kujenga na kupanua Shule Shikizi Kiunda iwe Shule ya Msingi kamili, inayojitegemea.

Tuma mchango wako wa fedha kwenye Akaunti ya Kijiji cha Kamguruki.

**Akaunti ya Benki:**
Benki: NMB
Akaunti Na: 30302300679
Jina la Akaunti: Kijiji cha Kamguruki

**TUENDELEE KUBORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA MUSOMA VIJIJINI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# HARAMBEE YA UJENZI WA SHULE SHIKIZI KIUNDA, MUSOMA VIJIJINI

January 8, 2024



*Hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu kwenye Shule Shikizi Kiunda ya Kijijini Kamguruki, Musoma Vijijini.*

**Tarehe ya Harambee**
Ijumaa, 12.1.2024
Saa 8 mchana

**Mahali:**
Kitongoji cha Kiunda
Kijijini Kamguruki

**Akaunti ya Benki:**
Benki: NMB
Akaunti Na: 30302300679
Jina la Akaunti: Kijiji cha Kamguruki

**Taarifa ya Kiunda:**
Shule Shikizi Kiunda inajengwa kwenye Kitongoji cha Kiunda, Kijijini Kamguruki, Kata ya Nyakatende.

Shule hii inatayarisha watoto wa vitongoji 3 kwenye masomo ya awali, baadae watoto hao wanaenda kuanza masomo ya Shule ya Msingi mbali na nyumbani kwao - tatizo la umbali mrefu wa kwenda masomoni.

**Ujenzi wa Shule Shikizi Kiunda:**
Wote tunakarabishwa kuchangia ujenzi wa shule hii kwa kushiriki HARAMBEE iliyoelezwa hapo juu, au kutuma mchango wako moja kwa moja kwenye Akaunti ya Kijiji cha Kamguruki.

**KARIBU TUBORESHE ELIMU VIJIJINI MWETU**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# WANANCHI WA KITONGOJI CHA GOMORA WAAMUA KUONGEZA KASI KWENYE UJENZI WA SHULE SHIKIZI YAO

October 6, 2023



*Wananchi wa Kitongoji cha Gomora waamua kuongeza kasi kwenye ujenzi wa Shule Shikizi yao*

Kitongoji cha Gomora ni moja ya vitongoji vitatu (3) vya Kijiji cha Musanja, Kata ya Musanja

Vitongoji hivi vitatu (3) vinayo Shule ya Msingi moja iliyojengwa Mwaka 1959 na Kanisa la Mennonite. Shule hiyo (S/M Musanja) kwa sasa ni ya Serikali.

**Matatizo makuu yanayowakabili wanafunzi wa S/M Musanja:**

*Umbali mrefu wa kutembea kwenda masomoni
*Mirundikano ya wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa
*Uchakavu wa miundombinu ya shule iliyofunguliwa Mwaka 1959

Harambee ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, kwa kushirikiana na Kamati ya Siasa ya Wilaya (CCM) iliyopigwa Ijumaa, 29.9.2023 ilikuwa ya mafanikio ya kuridhisha kwa kupata:

*Saruji Mifuko 150, ikiwemo 100 ya Mbunge wa Jimbo na 10 ya Diwani.
*Tsh milioni 3 za Halmashauri yetu.
*Fedha taslimu Tsh 306,000 zikiwemo Tsh 105,000 za Walimu Makada wa CCM.
*Mchanga tripu 3.

**ELIMU NI KIPAUMBELE CHETU CHA KWANZA KABISA, TAFADHALI NJOO TUCHANGIE UJENZI WA GOMORA SHULE SHIKIZI YA KIJIJI CHA MUSANJA**

Wana-Gomora waliahidi kuanza ujenzi leo, na kweli wamefanya hivyo - picha ya hapa (Ukurasa 42) inaonesha uchimbaji wa msingi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI

# WA

# MIRADI YA AFYA

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# WANAVIJIJI WANAENDELEA NA UJENZI WA ZAHANATI ZA VIJIJI VYAO

June 3, 2024



*Hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kataryo, Kata ya Tegeruka.*

Wanavijiji wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea na ujenzi wa zahanati za vijiji vyao kwa kushirikiana na Madiwani wao, na Mbunge wao wa Jimbo.

Jimbo la Musoma Vijijini lina Kata 21 zenye vijiji 68 na vitongoji 374. Kila kijiji kimedhamiria kujenga zahanati yake.

**Utaratibu unaotumika ni huu hapa:**

(i) Wanakijiji wanabuni mradi wa ujenzi wa zahanati ya kijiji

chao, wanatayarisha eneo la ujenzi, na wanapewa ushauri kutoka kwa Mhandisi wa Halmashauri yetu (Musoma DC).

(ii) Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo anapiga Harambee ya kuanza ujenzi wa zahanati ya kijiji husika.

(iii) Mbunge huyo anaendelea kushirikiana na wanakijiji kuchangia ujenzi wa zahanati inayojengwa hadi hapo Serikali itakapoanza kuchangia ukamilishaji wake.

(iv) Serikali hukamilisha ujenzi wa zahanati na kuweka vifaa tiba na wafanyakazi wanaohitajika.

Jimbo letu lina jumla ya Zahanati 29 zinazotoa Huduma za Afya. Kati ya hizo, 25 ni za Serikali na 4 ni za Binafsi.

Jimbo lina Vituo vya Afya sita (6) na Hospitali moja (1) ya Halmashauri/Wilaya.

**Zahanati 16 zinaendelea kujengwa:**
Vijiji vinavyojenga zahanati mpya ni hivi vifuatavyo: Burungu, Butata, Chanyauru, Chimati, Chirorwe, Kaburabura, Kakisheri, Kataryo, Kurukerege, Kurwaki, Kwikerege, Maneke, Mabuimerafuru, Nyabaengere, Nyambono na Nyasaungu.

**Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kataryo:**
Kijiji cha Kataryo ni moja ya vijiji vitatu vya Kata ya Tegeruka. Vijiji vingine ni: Mayani na Tegeruka. Kata hii inayo zahanati moja tu inayohudumia vijiji vyote, na imejengwa Kijijini Mayani.

Kijiji cha Kataryo kimeamua kujenga zahanati yake kwa kutumia nguvukazi na michango ya fedha za wanakijiji, na baadhi ya wadau wa maendeleo wa kijiji hicho.

Diwani wa Kata hiyo, Mhe Alpha Modikae Mashauri amechangia Saruji Mifuko 50, na amehaidi kuendelea kuchangia ujenzi huo.

Mbunge wa Jimbo ameanza kutoa michango yake, kwa kuanza na Saruji Mifuko 200, nae ataendelea kuchangia ujenzi huo.

**Akaunti ya Benki ya Kijiji cha Kataryo:**
Benki: NMB
Akaunti Na: 30302300302
Jina la Akaunti: Kijiji cha Kataryo

Wana-Kataryo wanaomba mchango wako uwasaidie kukamilisha ujenzi wa Zahanati yao kabla ya Disemba 2024. Tafadhali tuma mchango wako wa fedha kwenye Akaunti ya kijiji chao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KATA ISIYOKUWA NA KITUO CHA AFYA NA ZAHANATI HATA MOJA YAAMUA KUJENGA ZAHANATI MBILI

March 25, 2024



*Harambee ya ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mabuimerafuru.*

Kata ya Musanja yenye vijiji vitatu (3) haina Kituo cha Afya na haina Zahanati hata moja kwenye vijiji vyake. Vijiji hivyo ni: Mabuimerafuru, Musanja na Nyabaengere.

Hii ndiyo Kata pekee Jimboni mwetu yenye hali kama hiyo kwa upande wa Huduma za Afya!

Wanavijiji wa Kata hii wanalazimika kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita kumi (km 10) kwenda kupata Huduma za Afya kwenye Kata jirani ya Murangi (Kituo cha Afya cha Murangi).

**Zahanati ya Kijiji cha Nyabaengere:**
Zahanati hii inakaribia kuanza kutoa Huduma za Afya. Maombi ya kufungiwa umeme yamepelekwa TANESCO.

**Zahanati ya Kijiji cha Mabuimerafuru:**
Mbunge wa Jimbo la MusomaVijijini, Prof Sospeter Muhongo aliendesha Harambee ya ujenzi wa Zahanati ya kijiji hiki siku ya Jumatano, 20.3.2024.

**Matokeo ya Harambee hiyo:**
1. Fedha zilizopatikana: Tsh 1,350,000
2. Saruji Mifuko 59
3. Kondoo 2
4. Mbunge wa Jimbo: Saruji Mifuko 200 (mia mbili)

Kamati ya ujenzi iliundwa chini ya uongozi wa Ndugu Justine Joshua

**Michango kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wa Kata ya Musanja:**
Uchangiaji ufanyike kwa kutuma fedha za michango moja kwa moja kwenye Akaunti ya Kijiji ambayo ni:

Benki: NMB
Akaunti Na: 30310037402
Jina: Kijiji cha Mabuimerafuru

Viongozi wa CCM wa Kata na Matawi, na baadhi ya wananchi wa Kata ya Musanja walipewa vitabu viwili viwili vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 ndani ya vijiji vyote 68 vya Jimboni mwetu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KIJIJI CHA KABURABURA KIMEANZA KUJENGA ZAHANATI YAKE – TUWAUNGE MKONO

March 20, 2024



Wiki jana, uamuzi wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kaburabura ulifanywa na wanakijiji wenyewe.

Kamati ya ujenzi iliundwa, na sasa kazi zimeanza kwa kutumia nguvukazi za wanakijiji wenyewe - angalia picha.

Tafadhali tuwaunge mkono kwa kuchangia ujenzi wa Zahanati ya Wana-Kaburabura

**Tafadhali tuma mchango wako kwenye Akaunti ya Kijiji chao:**

Benki: NMB
Akaunti Na: 30302300684
Jina: Kijiji cha Kaburabura

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KISIWA CHA RUKUBA KIMEKAMILISHA UJENZI WA KITUO CHA AFYA

July 9, 2023



*Majengo ya Kituo cha Afya cha Kisiwa cha Rukuba, Musoma Vijijini.*

Kisiwa cha Rukuba kiko ndani ya Kata ya Etaro yenye vijiji vinne (Busamba, Etaro, Mmahare na Kisiwa cha Rukuba).

Kisiwa hiki cha Musoma Vijijini kina Shule ya Msingi yenye vyumba vya madarasa vya kutosha ikiwepo ziada ya vyumba viwili. Madawati yapo ya kutosha kwa wanafunzi wote. Ofisi mbili (2) za Walimu zipo.

Maktaba ya shule ipo. Kila Mwalimu amepatiwa makazi mazuri. Wana-Rukuba na Mbunge wao wa Jimbo wameanza ujenzi wa Sekondari hapo Kisiwani.

**Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Afya:**
*Wakazi wa Kisiwa cha Rukuba waliamua kupanua Zahanati yao iwe Kituo cha Afya.

*Upanuzi huo ulianza kutekelezwa kwa kutumia michango ya fedha na nguvukazi za wananchi na Mbunge wao, Prof Sospeter Muhongo.

**Tsh Milioni 500 kutoka Serikalini:**
*Wakazi wa Kisiwa cha Rukuba na Viongozi wao wanaishukuru sana Serikali kwa kuwapatia Tsh Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya hapo Kisiwani.

*Kituo cha Afya kimekalika na kiko tayari kutumika. Majengo manne (4) na miundombinu yake yaliyokamilika ni:
(i) Mama & Mtoto
(ii) Maabara
(iii)Upasuaji
(iv)Ufuaji

Jengo la OPD litatumika lile la Zahanati wakati Jengo jipya likiwa linakamilishwa.

**Ombi la Wafanyakazi & Vifaa Tiba:**
Wakazi wa Kisiwani Rukuba wanaiomba Serikali (TAMISEMI & Wizara ya Afya) iwapelekee Wafanyakazi na Vifaa Tiba ili Kituo hicho kianze kutoa huduma za Afya Kisiwani hapo - Wakazi wa hapo Kisiwani wanataka wapunguze sana kusafirisha wagonjwa mahututi na mama wajawazito kwenye mitumbwi kwenda Musoma Mjini kwa matibabu.

**SHUKRANI**
Wananchi wakazi wa Kisiwa cha Rukuba na Viongozi wote wa Musoma Vijijini wanaendelea kutoa shukrani zao za dhati kwa Serikali yetu na kwa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwapatia fedha za miradi ya maendeleo ikiwemo ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya huduma za afya vijijini mwao.

Tafadhali usiache kutembelea TOVUTI yetu ambayo ni: www.musomavijijini.or.tz

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# SHEREHE ZA MUUNGANO: VIONGOZI WA WILAYA WAPANDA MICHE YA MITI NA KUFANYA USAFI KIJIJINI KIGERA

April 30, 2024




*Leo, Watanzania wote tunasherehekea kwa furaha na amani tele ya miaka sitini (60) ya Muungano wetu.*

Jimbo la Musoma Vijijini lilikua na ratiba ya siku kadhaa za kupanda miti na kufanya usafi sehemu mbalimbali za vijijini mwetu ikiwa ni sehemu ya Sherehe za Muungano.

Tunamshukuru sana Mkuu wa Wilaya (DC) yetu ya Musoma, Mhe Dkt Khalfany Haule kwa kusimamia na kuongoza vizuri sana matukio yote ya sherehe za Muungano wilayani mwetu.

**Shule ya Msingi Ekungu, Kijijini Kigera (Etuma), Kata ya Nyakatende:**

Mhe DC wetu aliongoza upandaji wa miche ya miti ya matunda, mbao na kivuli kwenye shule hii.

Vilevile, kila mwafunzi aligawiwa miche mitatu ya kupanda na kutunza kwenye maeneo ya nyumbani kwao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# WAFUGAJI WA MUSOMA VIJIJINI WAENDELEA KUUNDA VIKUNDI VYA UCHUMI: KATA ZA IFULIFU NA NYAKATENDE ZAOMBA JOSHO LAO LA MWAKA 1956 LIBORESHWE

April 8, 2024



*Ziara ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo kijijini Kabegi, Kata ya Ifulifu.*

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alikaribishwa kutembelea josho na rambo la wafugaji wa Kata za Ifulifu na Nyakatende.

Josho wanalolitumia lilijengwa Mwaka 1956, na kwa sasa linahudumia ng'ombe zaidi ya elfu tano (5) kutoka vijiji saba vya Kata hizo mbili.

Wafugaji wa Kata hizo mbili wameanzisha vikundi kadhaa vya wafugaji, wauzaji maziwa na wakulima wa nyasi za malisho.

**Maombi makuu ya wafugaji hao:**

(i) Josho la Mwaka 1956 lililojengwa Kijijini Kabegi liboreshwe kwa kuziba nyufa, na liwe la kisasa.

(ii) Chanzo cha maji: rambo la Kijijini Kabegi limejaa tope na kingo za kuta zimebomoka hazipo.

Mbunge wa Jimbo ameahidi kufikisha maombi hayo Serikalini.

Vilevile, Mbunge huyo aliwagawia wanavijiji vitabu viwili viwili vinavyoelezea mafanikio makubwa yanayopatikana Jimboni mwetu kutokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025.

**Vyanzo vya mapato ya wananchi wa Jimboni mwetu ni:**

(i) Kilimo cha pamba, na cha mazao ya chakula (mihogo, mahindi, mpunga, viazi vitamu, alizeti, mbogamboga na matunda).

(ii) Uvuvi wa samaki ndani ya Ziwa Victoria na kwenye baadhi ya mito.

(iii) Ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku.

(iv) Uchimbaji wa madini, hususani dhahabu - wachimbaji wadogo wadogo.

(v) Biashara za aina mbalimbali

**KILIMO, UVUVI na UFUGAJI ni AJIRA KUU za Jimboni mwetu - tuendelee kuboresha mazingira na vitendea kazi vyake.**

# SIKU YA MISITU DUNIANI (THE INTERNATIONAL DAY OF FORESTS) – MUSOMA VIJIJINI WAISHEREHEKEA KWA KUPANDA MITI MASHULENI

March 23, 2024



*Matukio mbalimbali yaliyoelezwa hapo juu. Hapo ni Suguti Sekondari, Kijijini Suguti, Kata ya Suguti, Musoma Vijijini.*

Leo (21.3.2024) ni siku ya Umoja wa Mataifa (UN) ya kukumbushana umuhimu wa misitu ya aina zote.

UN ilipitisha azimio la siku hii (tarehe 21 Machi ya kila mwaka) kwenye Mkutano wake wa tarehe 28.11.2013

Kaulimbiu 2024: Misitu na Ubunifu (Forests and Innovations)

**Jimbo la Musoma Vijijini: Misitu na Ubunifu**
Kwa muda wa zaidi ya wiki mbili, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo akishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dkt Khalfany Haule, na Meneja wa Misitu (TFS) Wilaya, Ndugu Boniphace Kaberege wamekuwa wakigawa na kupanda mamia ya miche ya miti ya matunda, mbao na kivuli kwenye shule kadhaa za misingi na sekondari za Jimboni mwetu. Kampeni hii ni endelevu!

**Sherehe ya Uzinduzi wa Upandaji miti**
Jana, TFS Wilaya chini ya uongozi wa Ndugu Boniphace Kaberege ilitoa mafunzo ya umuhimu wa misitu kwa maisha na ustawi wa jamii zetu. Mafunzo hayo yalifanywa kwenye Sekondari ya Suguti.

Wanafunzi na Walimu wote wa Sekondari hiyo, wakiongozwa na Mkuu wao, Mwl Pendo Kaponoke walihudhuria mafunzo hayo.

Wanavijiji wa Kata ya Suguti (Vijiji 4 vya Chirorwe, Kusenyi, Suguti na Wanyere) walihudhuria, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata hiyo, Ndugu Alphonce Wambura

**"Environmental Ambassadors" - Suguti Sekondari”**
Wanufunzi 100 wa Sekondari hii wamekuwa, Mabalozi wa Mazingira chini ya Mwalimu wao wa Mazingira, Mwl Keneth Elias. Hawa wataongoza Kampeni ya upandaji na utunzaji miti ndani ya Kata na Suguti, na kwingineko Jimboni mwetu.

**Uzinduzi wa Upandaji na Utunzaji miti kwenye shule zote za Jimboni mwetu**

Jana, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini na Meneja wa TFS Wilaya walizindua kampeni endelevu ya upandaji na utunzaji wa miti kwenye shule zote za Jimboni mwetu. Uzinduzi huo ulifanyika Suguti Sekondari.

# KILIMO CHA UMWAGILIAJI NDANI YA BONDE LA BUGWEMA

October 6, 2023




***KILIMO CHA UMWAGILIAJI NDANI YA BONDE LA BUGWEMA***

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alidhamiria kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwenye bonde la Bugwema lililoko Musoma Vijijini.

Ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji ilianza kujengwa Mwaka 1974. Mradi ukasimama.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, ameiomba Serikali yetu ifufue mradi huo. Serikali imekubali na kwenye Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha (2023/2024) - kazi za, "feasibility studies & designing", zimeanza.

Jimbo letu lina mabombe makubwa mawili yenye vigezo vyote vya uanzishwaji wa kilimo kikubwa cha umwagiliaji - hayo ni mabonde ya Bugwema & Suguti.

**KILIMO CHA UMWAGILIAJI NDIYO SULUHISHO LA UHAKIKA KWA UPATIKANAJI WA CHAKULA CHA KUTOSHA & CHA BEI NAFUU NCHINI MWETU!**

Tafadhali usiache kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI YA MAJI

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# MAJI YA BOMBA KUTOKA ZIWA VICTORIA YAENDELEA KUSAMBAZWA MUSOMA VIJIJINI

August 9, 2023



*Ukaguzi wa miradi miwili ya Kata ya Bulinga, (i) mradi wa maji ya bomba, na (ii) maabara ya Sekondari ya Kata*

Jimbo la Musoma Vijijini lina Kata 21, Vijiji 68 na Vitongoji 374.

Vijiji vyetu vyote vina miradi ya maji ambayo iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Miradi ya maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria inatekelezwa kwa kasi kubwa Jimboni mwetu.

Jana, Mbunge wa Jimbo aliambatana na Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya ya Musoma Vijijini kukagua miradi miwili ya maji ya bomba inayotekelezwa na RUWASA. Utekelezaji wa miradi hiyo ni mzuri - Hongereni RUWASA.

**Mradi wa Kata ya Bwasi**
*Vijiji vitakavyonufaika na upatikanaji wa maji ya bomba ya mradi huu ni: Bwasi, Bugunda na Kome.

*Chanzo cha maji kiko ziwani kwenye Kitongoji cha Bujaga, Kijiji cha Bujaga, Kata ya Bulinga. Vijiji vitatu vya Kata ya Bulinga (Bujaga, Bulinga na Busungu) tayari vinapata maji ya bomba.

**Utekelezaji wa mradi huu:**
*Ujenzi wa Tenki la ujazo wa lita 150,000 unakamilishwa. Lipo kwenye Kitongoji cha Rugongo, Kijijini Bwasi.

*Bomba kuu la kusambaza maji limetandazwa kilomita 18 kati ya 31.5.

*Vituo vya kuchotea maji 25 kati ya 35 vimeishajengwa

*Gharama ya Mradi: Tsh 997,714,196 (Tsh 997.7m).

*Mradi ulianza Februari 2023, utakamilishwa kabla ya tarehe 30.10.2023.

**Mradi wa Chumwi-Mabuimerafuru**
Mradi huu unaanzwa kutekelezwa kwenye Vijiji vya Chumwi (Kata ya Nyamrandirira) na Mabuimerafuru (Kata ya Musanja), baadae utapanuliwa na maji yatasambazwa kwenye vijiji vyingine vya Kata hizo mbili.

**Utekelezaji wa mradi huu:**

*Chanzo cha maji ya mradi huu kiko ziwani kwenye Kitoji cha Nyachumwi, Kijijini Chumwi.

*Ujenzi wa Tenki la ujazo wa lita 300,000 unakamilishwa. Liko kijijini Mabuimerafuru.

*Bomba kuu la kusambaza maji limetandazwa umbali wa kilomita 13 kati ya 24.24

*Vituo vyote 17 vya kuchotea maji tayari vimejengwa

*Gharama ya Mradi ni Tsh bilioni 1.6

*Mradi huu ulianza kutekelezwa Februari 2023, utakamilika kabla ya tarehe 30.10.2023.

**Kero na matatizo ya wanavijiji:**

Wanavijiji walipata muda wa kutosha wa kuwasilisha kero na matatizo yao. Majibu yalitolewa na Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo. Maswali yaliyohusu Chama yalijibiwa na Mwenyekiti Ndg Denis Ekwabi na Katibu Ndg Valentine Maganga.

Kero na matatizo yaliyowasilishwa yalipata majibu ya uhakika na ya ukweli, waulizaji waliridhika.

Vilevile, Maabara za masomo ya sayansi ya Bulinga Sekondari yalitembelewa. Sekondari hii kwa sasa inazo maabara mbili

zilizokamilika na zinatumika (Chemistry & Biology). Ujenzi wa Maabara ya Physics unakamilishwa.

**SHUKRANI**

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini na Viongozi wao wa ngazi zote wanaishukuru sana Serikali, chini ya uongozi mzuri wa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia fedha za utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo - ahsanteni sana!

**Musoma Vijijini, TUNAFANIKIWA!**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI

# WA

# MIRADI YA UJENZI WA BARABARA

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# ZIARA YA WAZIRI MKUU MUSOMA VIJIJINI: SERIKALI KUENDELEA KUJENGA KWA KIWANGO CHA LAMI BARABARA LA MUSOMA-MAKOJO-BUSEKERA (Km 92)

March 5, 2024




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa amewaeleza wana-Musoma Vijijini kuhusu uamuzi wa Serikali kuendelea kutoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini mwao.*

Waziri Mkuu aliyasema hayo kwenye mkutano wake wa hadhara uliofanyika Kijijini Bwai Kwitururu, Musoma Vijijini siku ya Alhamisi, tarehe 29.2.2024

**Barabara kuendelea kuwekewa lami:**

Serikali imesema itaendelea kulijenga barabara letu kuu na muhimu la Musoma-Makojo-Busekera lenye urefu wa kilomita 92 kwa kiwango cha lami. Tuzingatie yafuatayo kutoka Serikalini:

(i) Kilomita 5 zimeishawekewa lami.
(ii) Barabara limo kwenye Bajeti ya mwaka huu (2023/2024).
(iii) Kibali kimetolewa barabara litangazwe na Mkandarasi apatikane, na aendelee na ujenzi.

**Shukrani:**
Wana-Musoma Vijijini tunaendelea kuishukuru Serikali yetu, chini ya uongozi mzuri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi za kufadhili miradi ya maendeleo vijijini mwetu.

Tunamshukuru sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Tanzania, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kututembelea Jimboni mwetu, na kwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo ambayo ni kielelezo cha mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UTAMADUNI
# NA
# MICHEZO

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# MBUNGE WA JIMBO ANUNUA TRACK SUITS 100 NA JEZI 16 KWA AJILI YA TIMU YA UMITASHUMTA YA MUSOMA VIJIJINI

May 31, 2024



*Wanafunzi wakiwa mazoezini kwenye Shule ya Msingi Suguti, Kijijini Suguti, Kata ya Suguti.*

Timu ya UMITASHUMTA ya wanafunzi wa Shule za Msingi za Musoma Vijijini wako kambini wakifanya mazoezi yakiwa ni kwa ajili ya maandalizi yao ya mashindano ya UMITASHUMTA Mkoa wa Mara.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo amechangia ushiriki wa wanafunzi wetu kwenye mashindano hayo kwa kununua:
*Track suits 100
*Jezi 16 za wachezaji wa mpira wa miguu.

**Michezo na Utamaduni:**
Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 inaelezea umuhimu wa michezo na utamaduni kwa Taifa letu.

Michezo na Utamaduni ni moja ya vipaumbele vikuu vitano (5) vya Jimbo letu, na inatekelezwa vizuri.

Tunawatakiwa wanafunzi wetu ushindi mzuri kwenye mashindano ya UMITASHUMTA

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MENGINEYO

***(30 Juni 2024 – 1 Julai 2023)***

# MAJI YAONGEZEKA ZIWA VICTORIA: BAADHI YA KAYA KISIWANI RUKUBA ZAHIFADHIWA KWENYE KITUO CHA AFYA

May 7, 2024



Mvua zinaendelea kunyesha, na maji Ziwa Victoria yanaendelea kuongezeka.

Siku ya leo siyo nzuri Kisiwani Rukuba, Kaya ya Etaro kwani kaya tano (5) hazina makazi zimehifadhiwa kwenye Kituo cha Afya cha hapo Kisiwani. Maji yanaendelea kuongezeka, na makazi ya kaya nyingine thelathini na mbili (32) yako hatarini.

**Kuongezeka kwa maji ndani ya Ziwa Victoria**

Mifano hii miwili itatuonyesha jinsi maji yalivyoongezeka ndani ya Ziwa Victoria kwa upande wa Wilaya ya Musoma:

i.) **Kisiwani Rukuba, Kata ya Etaro:**
Waathirika wa Kisiwani humo wanasema, "maji yamewafuata" kwa takribani mita 30-40 hadi kwenye makazi yao.

ii.) **Mji wa Musoma:**
Waathirika wanaoishi karibu na ufukwe wa Ziwa Victoria wanasema "maji yamewafuata kwa takribani mita 5" hadi kwenye makazi yao.

iii.) **Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria, Mwanza:**
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo amewasiliana na wataalamu wetu walioko kwenye Ofisi hiyo, na kupata jibu lifuatalo:

Maji yameongezeka kwa kiasi cha wastani wa kina cha mita 1.65

**USHAURI:**
Wananchi wanaoishi karibu na ufukwe wa Ziwa Victoria wanalazimika kufuata ushauri watakaopewa na viongozi mbalimbali, kwa ajili ya kuepuka mafuriko au ongezeko la maji ndani ya Ziwa Victoria.

Vilevile, wananchi wanahimizwa kufuatilia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa kila siku na wataalamu wa hali ya hewa wa TMA.

Ziwa Victoria lenye kawaida ya ujazo wa maji wa takribani kilomita za ujazo 2,424 (2,424 cubic kilometres), kwa sasa maji yaongezeka sana! Tuchukue tahadhari kubwa!

# MVUA KUBWA NA UPEPO MKALI VYALETA MAAFA KWA WATU 685 KIJIJINI LYASEMBE

April 12, 2024



*Mkuu wa Wilaya ya Musoma (DC), Dkt Khalfany Haule (na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya), na wananchi waathirika wakiwa kwenye eneo la maafa Kijijini Lyasembe. Hiyo ilikuwa siku ya Jumamosi, 6.4.2024.*

Ijumaa, 5.4.2024 mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali vilileta maafa makubwa Kijijini Lyasembe, Kata ya Murangi.

**Jumla ya watu walioathirika ni: 685**
Watoto 384
Watu wazima 301

**Jumla ya majengo yaliyoharibika:**
(i) Nyumba zilizobomoka (17):
17 za wanakijiji.

(ii) Nyumba zilizoezuliwa mapaa (61):
59 za wanakijiji, 2 vyumba vya madarasa ya S/M Lyasembe

**Miti ya shule iliyoharibiwa na upepo mkali (40):**
Miti mikubwa iliyong'olewa mizizi: 28
Miti iliyovunjiwa matawi makubwa: 12

**MICHANGO KWA WAATHIRIKA**

(i) Serikali ya Kijiji inaomba misaada ya aina mbalimbali husυsani vifaa vya ujenzi (saruji, mabati, mbao na misumari).

**Fedha za michango zipelekwe kwenye Akaunti ya Kijiji ambayo ni:**

Benki: NBM
Akaunti Na: 30302300012
Jina: Kijiji cha Lyasembe

(ii) Shule ya Msingi Lyasembe
Shule hii iliyofunguliwa Mwaka 1975, kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 811, na walimu 10.

Shule hii ina jumla ya vyumba vya madarasa 10, kati ya hayo matano (5) ni chakavu. Mawili kati ya hayo chakavu yameezuliwa mapaa! Mahitaji halisi ya shule hii ni vyumba vya madarasa 21, na nyumba za walimu 10 (two in one).

Bodi ya shule imeamua kuhamasisha wanakijiji wajenge madarasa mapya wakianza na jengo lenye vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja.

**Fedha za michango zipelekwe kwenye Akaunti ya Shule ambayo ni:**

Benki: NMB
Akaunti Na: 3033700134
Jina: Shule ya Msingi Lyasembe

**Wazaliwa wa Kata ya Murangi:**
Wanavijiji wa Kata ya Murangi (Kata ina vijiji viwili - Lyasembe na Murangi) wanaomba Wana-Murangi wajitokeze kuchangia waathirika wa maafa yaliyoelezwa hapo juu.

Wadau wengine wa maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini wanaombwa kuchangia waathirika wa maafa yaliyoelezwa hapo juu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MRADI WA UFUNGAJI WA MINARA MIPYA YA MAWASILIANO WAANZA KUTEKELEZWA JIMBONI MWETU

March 16, 2024



*Mnara mpya wa VODA uliojengwa ndani ya eneo la Bugwema Sekondari, Kijijini Masinono.*

Maombi yetu ya kuomba kuboreshewa mawasiliano ya simu, intaneti, n.k. yaanza kutekelezwa.

Mnara mpya wa VODA umejengwa Kijijini Masinono ndani ya eneo la Bugwema Sekondari. Wanakijiji wanakiri kwamba mawasiliano kupitia mtandao wa VODA kwa sasa ni mazuri sana.

Mbunge wa Jimbo anaendelea kufuatilia maombi yetu ya kuongezewa idadi ya minara ya mawasiliano vijijini mwetu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI: VITABU VINAVYOELEZEA UTEKELEZAJI YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM (2020-2025) VINASAMBAZWA

February 17, 2024



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa akipokea vitabu kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo.*

**Bungeni:**
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, amemkabidhi Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa vitabu viwili (2) vinavyoelezea miradi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025, ndani ya Jimbo letu.

Mbunge huyo anaendelea kuchapisha vitabu vingine hadi mwaka ujao, 2025.

**Tovuti ya Jimbo letu:**
www.musomavijijini.or.tz

Inazo taarifa muhimu za maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini. Vitabu hivyo navyo viko kwenye Tovuti hiyo.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# LEO BUNGENI-JUMATANO, 7.2.2024

February 9, 2024





*Prof Sospeter Muhongo ametoa ushauri wa kuboresha elimu yetu iendane na matakwa ya ukuaji wa uchumi wa wakati huu.

*Prof Muhongo ameonyesha umuhimu wa kuwekeza kwenye masomo ya sayansi na teknolojia, na kutolea mfano nchi ya India ambayo mwaka jana (2023) pato lake la Taifa (GDP), lilikuwa la tano (5) Duniani lenye US Dollar Trilioni 3.7, sawa na 3.7% ya GDP ya Dunia.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UGAWAJI WA VITABU VINAVYOELEZEA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM (2020-2025) UMEANZA

January 19, 2024




Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo ameanza kugawa VITABU VIWILI (Volumes III & IV) vya utekelezaji wa Ilani yetu ya sasa (2020-2025)

Vitabu hivi kama vile viwili (Volumes I & II) vya Ilani ya 2015-2020, vinataja majina ya wachangiaji wa miradi inayotekelezwa Jimboni mwetu.

Wanavijiji wa Jimbo la Musoma Vijijini, Viongozi wa ngazi mbalimbali za Chama (CCM) na Serikali wamepewa nakala ya vitabu hivi viwili ambavyo vinagawiwa bure.

Ugawaji unaendelea, utafika hadi kwenye Vitongoji. Uchapishaji wa vitabu vipya unaendelea - Miradi ya maendeleo ya wananchi wa Musoma Vijijini ni mingi.

Wiki ijayo Vitabu 2 (Volumes III & IV) vitawekwa kwenye Tovuti ya Jimbo:
www.musomavijijini.or.tz

Tembelea Tovuti hiyo ya Jimbo letu usome vitabu hivyo na vile vya awali (Volumes I & II, Ilani ya 2015-2020)

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MISIBA KISIWANI RUKUBA: DHORUBA KUBWA YAVUNJA MTUMBWI NA KUSABABISHA VIFO VITATU

January 17, 2024



*Maombolezo yanaendelea pembeni mwa Ziwa Victoria, Kisiwani Rukuba.*

Tunasikitika kupoteza ndugu zetu 3 waliokufa maji siku ya Jumapili usiku kuamkia Jumatatu (jana, 15.1.2024). Dhoruba kubwa ilivunja mbao za mtumbwi na maji yakazamisha mtumbwi huo.

Mtumbwi ulikuwa na wavuvi 4: mmoja amesalimika (kwao Musoma Mjini) na watatu wamekufa maji (2 kwao Maneke & 1 kwao Nyegina)

**Utafutaji wa miili ya marehemu:**

*Ajali ilitokea eneo la mbali kutoka Kisiwani Rukuba - mwendo wa takribani masaa matatu kuelekea Kisiwa cha Goziba (Bukoba)

*Mitumbwi 10 inaanza kazi ya kutafuta miili hiyo kesho. Mafuta yanayohitajika ni lita 500 au zaidi.

**Michango ya mafuta ya kutafuta waliokufa maji**
(i) Wana-Rukuba wamejichangia lita 300
(ii) Mbunge wa Jimbo amechangia lita 200

**Maombi ya michango kutoka vyanzo vingine:**
Mahitaji ya misiba hii mitatu ni mengi na makubwa. Tafadhali changia misiba hii kwa kutuma fedha kwenye Akaunti ya Kisiwa/Kijiji cha Rukuba.

Benki: NMB
Akaunti Na.: 30302300701
Jina la Akaunti: Serikali ya Kijiji cha Rukuba

Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na matumaini mema wanafamilia wa marehemu hao watatu. Tuendelee kuwafariji wafiwa!

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# PROF MUHONGO AENDELEA KUJENGA UZIO (UKUTA) KWENYE MAKABURI YA MUSOMA MJINI

July 24, 2023



*Uzio unajengwa kwa kuhakikisha kwamba makaburi yaliyoko nje kidogo ya eneo la mpaka wa makaburi yanaingizwa ndani ya uzio.*

Makaburi yaliyo kwenye eneo la Kanisa la Mennonite la Kitaji, Musoma Mjini yalikuwa hayana uzio (ukuta). Utunzaji wake ni mgumu sana.

Wazo la kujenga uzio kwenye makaburi hayo lilitolewa na Profesa Sospeter Muhongo. Michango ilikaribishwa na kutolewa kwa kusuasua sana, na ikawa ni midogo mno! Michango ilipelekwa kwenye Kanisa lenye makaburi. Ujenzi ukaanza kwa kusuasua sana. Malumbano yakaanza kujitokeza.

Mtoa wazo la ujenzi, Prof Muhongo akaamua yafuatayo:

*Michango isimame, tuepuke malumbano.
*Ujenzi uendelee kwa ufadhili wake, yaani wa Prof Sospeter Muhongo.

**Maendeleo ya ujenzi:**
*Eneo lenye makaburi limesafishwa kwa kukata nyasi na vichaka.

*Mafundi wengine wamewekwa kufanya kazi ya ujenzi.

*Uzio unajengwa kwa kuhakikisha kwamba makaburi yaliyoko nje kidogo ya eneo la mpaka wa makaburi yanaingizwa ndani.

Sospeter Muhongo
Jumapili, 23.7.2023

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# MWENGE WA UHURU MUSOMA VIJIJINI: HUDUMA ZA AFYA ZAENDELEA KUBORESHWA NA KUIMARISHWA

July 15, 2023



*Picha ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndugu Abdalla Shaibu Kaim na Timu yake yote wameipongeza sana Serikali na Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa michango mikubwa ya kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Musoma Vijijini.*

Vilevile, Wananchi na Viongozi wao wa Chama na Serikali wa Musoma Vijijini wamepongezwa sana kwa kazi nzuri wazifanyazo kwenye utekelezaji ya miradi ya maendeleo ya vijijini mwao.

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374.

Wanavijiji na Viongozi wao mbalimbali wanaendelea kushirikiana na Serikali kujenga na kuboresha miundombinu ya utoaji wa Huduma za Afya kwenye maeneo yao ya vijijini, kama ifuatavyo:

**(I) Hospitali ya hadhi ya Wilaya (1):**
*Inaendelea kujengwa kwenye Kitongoji cha Kwikonero, Kijijini Suguti. Huduma ndogo ndogo (OPD) zimeanza kutolewa hapo.

**(II) Vituo vya Afya (6):**
*Vituo vya Afya vinavyotoa Huduma za Afya ni vitatu (3) - Murangi, Mugango na Bugwema

*Vituo vipya vya Afya vinavyosubiri kupewa wafanyakazi na vifaa tiba ni vitatu (3) - Makojo, Kiriba na Kisiwani Rukuba (inatoa huduma kwa hadhi ya Zahanati)

**(III) Zahanati (41):**
*Zahanati zinazotoa Huduma za Afya ni ishirini na nne (24) - Bugoji, Bugunda, Bukima, Busungu, Bwai Kwitururu, Chitare, Etaro, Kiemba, Kigera Etuma, Kiriba, Kome, Kurugee, Kwikuba, Masinono, Mayani, Mmahare, Mwiringo, Nyakatende, Nyambono, Nyegina, Rusoli, Seka, Suguti na Wanyere.

*Zahanati Binafsi zinatoa Huduma za Afya ni nne (4) - Bwasi (SDA), Mji wa Huruma (Katoliki), Kwibara (KMT) na Rwanga (KMT).

*Zahanati Mpya zinazojengwa ni kumi na tatu (13) - Burungu, Butata, Chanyauru, Chimati, Chirorwe, Kaburabura, Kakisheri, Kurukerege, Kurwaki, Maneke, Mkirira, Nyambono na

Nyasaungu.

(IV) **Magari ya kusafirisha Wagonjwa (Ambulances)**

*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ameleta na kugawa magari matano (5) ya Wagonjwa kama ifuatavyo: Kituo cha Afya cha Murangi (ambulance kubwa ya kisasa), Zahanati za vijiji vya Masinono (sasa Kituo cha Afya cha Bugwema), Kurugee, Nyakatende na Mugango (sasa Kituo cha Afya cha Mugango).

**Mwenge wa Uhuru Kijijini Kurwaki**

Jana, Jumatatu, 10.7.2023, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndugu Abdalla Shaibu Kaim aliweka Jiwe la Msingi kwenye Zahanati ya Kijiji cha Kurwaki iliyoanza kujengwa na Wananchi wa Kijiji hicho wakishirikiana na Mbunge wa Jimbo, Madiwani na Viongozi wao wengine.

Serikali imeanza kuchangia kwa kutoa Tsh Milioni 50 kwenye ujenzi wa Zahanati hii.

**Mwenge wa Uhuru Jimboni mwetu:**

*Mkuu wa Wilaya (DC) yetu, Dr Khalifan Haule na Mwenyekiti wa CCM Wilaya yetu, Ndugu Denis Ekwabi, na Timu zao, wanapongezwa sana kwa kusimamia na kuratibu mbio za Mwenge Jimboni mwetu kwa mafanikio makubwa sana - Ahsanteni sana!

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

**HITIMISHO**

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 unaenda vizuri Jimboni mwetu, na mafanikio yake yanaonekana na kuthaminiwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Wanavijiji wanashirikiana na Serikali yao ya ngazi mbalimbali kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji ya jamii zao.

Taarifa hii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo letu ni ya mwaka mmoja wa fedha, yaani 1 Julai 2023 hadi 30 Juni 2024. Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa Jimboni mwetu kwa kipindi hiki iliibuliwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025), ambamo ndimo tulitoa vipaumbele vyetu vitano vya maendeleo.

Miradi yetu ya maendeleo ni endelevu, kwani inaibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano ambavyo navyo ni endelevu, na nyenzo kuu za utekelezaji wake nazo zinaendelea kuhitajika kwa ustawi wa jamii yetu.

Vipaumbele vyetu ni: (i) elimu, (ii) afya, (iii) kilimo, uvuvi na ufugaji, (iv) tabianchi na mazingira, na (v) michezo na utamaduni.

Nyezo kuu zinazohitajika kwenye utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vyetu ni maji, umeme, barabara, vyombo vya

usafirishaji na mawasiliano, rasilimali watu na taasisi za fedha na uchumi.

Ahadi zilizotolewa Jimboni mwetu na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali yake, chini ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ziliendelea kutekelezwa ikiwemo ahadi ya ujenzi wa barabara la Musoma-Makojo-Busekera (km 92) kwa kiwango cha lami.

Ahadi za Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, zimetekelezwa na kuvuka malengo yaliyowekwa kwa mwaka huu mmoja (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023). Michango ya Mbunge huyu ni mingi na mikubwa kama inavyoainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, anaendelea kushirikiana kwa ukaribu sana na wananchi, viongozi wa Chama (CCM) na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye utekelezaji wenye mafanikio makubwa wa Ilani ya Uchaguzi (2020-2025) Jimboni mwao.

Vilevile, Mbunge huyu anaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Chama chetu (CCM) kwa ngazi zote, yaani, kuanzia Matawi, Kata, Wilaya (Musoma Vijijini), Mkoa (Mara) hadi Taifa (Tanzania).

**SHUKRANI**

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini na viongozi wao wa ngazi za Vitongoji (374), Vijiji (68) na Kata (21), na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, wanatoa shukrani nyingi za dhati kwa Mwenyekiti wa CCM Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa uwezeshaji na uongozi wake mzuri kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023).

Rais wa Serikali ya Mapinduizi ya Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mhe Dkt Hussein Ali Mwinyi anapewa shukrani nyingi kwa ushauri wake mzuri anaoutoa kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023).

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Philip Isdor Mpango anapewa shukrani nyingi kwa ushauri na ufuatiliaji mzuri anaoufanya kwenye miradi ya maendeleo ya Jimboni mwetu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Abdalrahman Kinana, na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Ndugu Daniel Chongolo nao wanapewa shukrani nyingi za dhati kwa usimamizi wao mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu (CCM) kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023).

Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, na viongozi wengine wote wa ngazi mbalimbali za Serikali yetu wanapewa shukrani nyingi za uwezeshaji na ushirikiano wao kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023). Utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Jimboni mwetu) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ulisimamiwa vizuri ki-Serikali na Wakuu wawili wa Mkoa wa Mara wa wakati huo ambao ni Mhe Meja Jenerali Suleiman Mzee na Mhe Saidi Mtanda.

Mkuu wa Wilaya yetu ya Musoma, Mhe Dkt Khalfany Boniface Haule anapongezwa na kupewa shukrani nyingi za dhati kwa uchapaji kazi wake mzuri wenye ufuatialiji na usimamiaji makini wa miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa Jimboni mwetu.

Shukrani nyingi pia zinatolewa kwa viongozi mbalimbali wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kuanzia ngazi za Tawi, Kata, Wilaya hadi Mkoa (Mara). Baadhi yao ni Mlezi wa Mkoa ki-Chama, Ndugu Abdulrahman Kinana, M-NEC Mkoa, Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Mkoa, Ndugu Patrick Chandi Marwa, Katibu wa Mkoa, Ndugu Langaeli Akyoo. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Denis Ekwabi na Katibu wa Chama Wilaya, Ndugu Valentine Maganga.

Waheshimiwa Madiwani wote 28 wakiwemo wa Viti Maalumu, na wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) wanapewa shukrani za dhati kwa utimizaji wa wajibu wao kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu (CCM) ndani ya mwaka huu mmoja.

Shukrani nyingi inapewa RUWASA kwa kufufua miradi iliyokwama kwa miaka kadhaa, na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya usambazaji wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria, na uchimbaji wa visima virefu vya maji vijijini mwetu.

TARURA na TANROADS wanaendelea kuboresha barabara zetu ambazo zinapitika kwa urahisi kwa majira yote ya mwaka.

Vyanzo vya fedha na vifaa vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini mwetu iliyobuniwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya mwaka huu mmoja wa fedha (30 Juni 2024 - 1 Julai 2023), ni vingi vikiwemo: Serikali Kuu na miradi yake kama vile EQUIP, EP4R, Wadau wa Maendeleo (PCI Tanzania na BMZ Germany), Benki za NBC, NMB na CRDB.

Mbunge wa Jimbo ametoa michango mingi na mikubwa kuchangia utekelezaji wa miradi inayoelezwa ndani ya kitabu hiki. Wanavijiji wamechangia nguvukazi na fedha taslimu. Baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini wametoa michango yao na majina yao yametajwa ndani ya kitabu hiki. Michango kutoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ya Jimboni mwetu imeainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo anapenda kuwashukuru watu mbalimbali wenye fani mbalimbali anaofanya nao kazi za Jimbo la Musoma Vijijini. Orodha ni ndefu na kwa uwakilishi wao anamshukuru Mtendaji Mkuu (Webmaster) wa Tovuti ya Jimbo letu (www.musomavijijini.or.tz), Dkt Isack Kambira.

Wengine wanaopewa shukrani ni Waandishi wa Habari wakiwakilishwa na Ndugu Sadick Hunga, Mussa Makali na Shomari Binda. Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wanapewa shukrani nyingi kwa kazi zao nzuri - hao ni Vaileth Peter, Benjamin John na Abdallah Juma.

Shukrani za kipekee na za muhimu sana zinapewa WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao kwa utashi wao wenyewe wameamua kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025. Miradi ya maendeleo inayotekelezwa vijijini mwao inabuniwa, inachangiwa (nguvukazi na fedha tasilimu), inatekelezwa na inatunzwa na wao wenyewe.

Vilevile, wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanashirikiana vizuri sana na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa makubwa ya ukuaji, uimarikaji wa uchumi na ustawi wa Jimbo letu la Musoma Vijijini.

**Kitabu hiki kimetayarishwa na:**
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini

**Prof. Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo**
Officier, Ordre des Palmes académiques
FGSAf, FAAS, MASSAf, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE,
FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol

**Homepage/Tovuti:**
www.musomavijijini.or.tz

**Telephone/Simu:**
+255 754 400 800

**Date/Tarehe:**
30 Juni 2024